

## ii. المَدُّ اللَّازِمُ الْكَلِمِيَّ الْمُخَفَّفُ Al-Madd Al-Laazim Al-Kalimiyyi Al-Mukhaffaf

Huitwa الْكَلِمِيَّ (ya neno) kwa vile inatokana na neno. Huitwa الْمُخَفَّفُ (khafifu) itakapokuja baada ya herufi ya madd herufi saakin isiyo na shaddah kwa maana, hapatoeki idghaam. Katika riwaayah ya Hafsw 'an 'Aaswim hakuna isipokuwa mara mbili pekee katika neno moja tu nalo ni ءَالْكُنْ katika Swurat Yuwnus:

أَنْتُمْ إِذَا مَا وَقَعَ ءَامَنْتُمْ بِهِ ءَالْكُنْ وَقَدْ كُنْتُمْ بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥١﴾<sup>1</sup>

**Bonyeza usikilize**

ءَالْكُنْ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾<sup>2</sup>

---

<sup>1</sup>Yuwnus (10: 51)

<sup>2</sup> Yuwnus (10: 91)